

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOPITIWA NA MWENGE WA UHURU, 2019**

### **A. UTANGULIZI**

Wilaya ya Chemba ina jumla ya wakaazi 235,711 ambao ni sawa na 11.3% ya wakazi wote wa Mkoa wa Dodoma. Vilevile Wilaya ya Chemba ina ukubwa wa eneo 7,653 ambazo ni sawa na 18.5% ya ukubwa wa eneo la Mkoa wa Dodoma. Hali ya Uchumi ya Wilaya hii inategemea zaidi kilimo na Mifugo. Hivyo, sisi wananchi wa Wilaya hii tunadhamiria kwa dhati kuondokana na umasikini kwa kupanua na kuboresha shughuli za kilimo cha mazao ya chakula, biashara ,Mifugo sambamba na kuboresha huduma katika Sekta za Afya, Maji, Ujenzi, Maliasili, Mazingira, Biashara, Ukusanyaji mapato, Elimu ya Msingi na Sekondari

Mwenge wa Uhuru utakimbizwa jumla ya kilomita 314 katika Wilaya ya Chemba na kuweka jiwe la Msingi Miradi ya Maendeleo miwili na kuzindua Miradi ya Maendeleo mitatu yenye thamani ya ya Shilingi za Kitanzania **Bilioni moja milioni mia tano themanini na nne laki nane kumi na tisa elfu mia tano sitini na tatu na senti ishirini na mbili tu (1,584,819,563.22)**

### **B. MIRADI ITAKAYOPITIWA NA MWENGE WA UHURU**

#### **1. UWEKAJI JIWE LA MSINGI UJENZI WA JENGO LA OFISI YA WATHIBITI UBORA WA SHULE**



Ujenzi wa Ofisi ya Wathibiti Ubora wa Shule ulianza rasmi Juni 2019, ikiwa ni miongoni mwa Wilaya zilizopokea fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Wathibiti Ubora waa Shule kutoka Serikali Kuu kupitia mpango wa lipo kwa Matokeo yaani EP4R.

Lengo la Mradi huu ni kuhakisha wadhhibiti ubora wa elimu Wilaya ya Chemba wanapata huduma ya utawala bora pamoja kuwezesha mazingira bora ya kufanyia kazi.. Mpaka sasa kazi za ujenzi wa jengo lenye ukumbi mmoja na vyumba sita, mfumo wa maji, mfumo wa umeme, samani za ukumbi mmoja na Ofisi sita, vifaa vya mawasiliano na maengesho ya magari zinaendelea.

Mradi huu utawanufaisha watumishi wa Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na wadau mbalimbali wa masuala ya elimu katika Wilaya ya Chemba pamoja na kuongeza usimamizi wa shule kwa wathibiti ubora.

Tunaishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na **MH. RAIS DKT. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI** kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha Ujenzi wa mradi huu.

## **2. UZINDUZI WA MRADI WA MAJI KIJIKI CHA MONDO**



Mradi huu ni mmojawapo ya miradi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya kuwapatia wananchi wa Kata ya Mondo huduma ya Maji safi na salama.

Lengo la Mradi huu ni kuhakikisha jamii ya Kijiji cha Mondo inapata huduma ya maji safi na salama katika umbali mfupi.

Mradi huu umegharimu kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi **673,898,236/=** Chanzo cha fedha za mradi ni Serikali kuu.

Mradi huu unafaida kwa wananchi wote waishio Kijiji Cha Mondo, mradi huu unanufaisha wakazi wapatao **4,731** wa kijiji cha Mondo.

Mradi huu unasaidia wananchi waishio Kijiji cha Mondo kupata Maji kwa umbali mfupi kama Sera ya Maji ya mwaka 2002 inavyotaka.

Tunaishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na **MHE. RAIS DKT. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI** kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha Ujenzi wa mradi huu.

### **3. UZINDUZI WA MRADI WA MAJI KIJIKI CHA PONGAI**



Mradi huu ni mmojawapo ya miradi ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya kuwapatia ya kuwapatia wananchi wa Kata ya Mondo huduma ya Maji safi na salama.

Lengo la Mradi huu ni kuhakikisha jamii ya Kijiji cha Pongai inapata huduma ya maji safi na salama katika umbali mfupi.

Mradi huu umegharimu kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi **332,242,992.22/=** fedha kutoka Serikali kuu.

Mradi huu unafaida kwa wananchi wote waishio Kijiji Cha Pongai, mradi huu unanufaisha wakazi wapatao **1,802** wa kijiji cha Pongai.

Tunaishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na **MH. RAIS DKT. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI** kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha Ujenzi wa mradi huu.

#### 4. UZINDUZI WA MRADI WA UJENZI WA CHUMBA CHA DARASA FARKWA SEKONDARI



Shule ya Sekondari Farkwa ni moja ya Shule zenye kidato cha tano na sita katika Wilaya ya Chemba. Katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa Mei mwaka 2018 ilianzisha ujenzi wa chumba cha darasa ambao ulikamilika Agosti 208.

Lengo la mradi huu ni kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi ikiwa ni mkakati wa Mpango Maalum wa Elimu wa Lipa kulingana na Matokeo (EP4R). Kwa sasa kazi ya ujenzi wa darasa imekamilika na utengenezaji wa madawati 40 umekamilika.

Mradi huu umegharimu kiasi cha fedha za kitanzania **21,046,170/=**. Kutoka Serikali Kuu kupitia Mpango wa Lipa kulingana na Matokeo (EP4R).

Tunaishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na **MH. RAIS DKT. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI** kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha Ujenzi wa mradi huu.



## 5. MRADI WA KITUO CHA AFYA KWAMTORO



Kituo cha Afya Kwamtoro ni moja kati ya vituo vya Afya vitatu (3) ambavyo vimepokea fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya. Kituo hiki kinahudumia wakazi wa Tarafa ya Kwamtoro na maeneo jirani.

Lengo la Mradi huu ni kusogeza na kuboresha huduma za afya karibu na jamii na kuongeza huduma ya mama na mtoto kwa wakazi wa Tarafa ya Kwamtoro. Kwa sasa kazi ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, jengo la maabara, jengo la upasuaji na jengo la kuhifadhia maiti umekamilika.

Mradi huu umegharimu kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi **405,580,000/=** kwa mchanganuo ufuatao:

- Serikali Kuu **Tsh 400,000,000/=**
- Jamii imechangia nguvu kazi **Tsh 5,580,000/=**

Tunaishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na **MH. RAIS DKT. JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI** kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha Ujenzi wa mradi huu.